Teofilo Kisanji University
TEKU Journal of Interdisciplinary Studies (TJIS)
https://www.teku.ac.tz/tjis.php

MAKALA HALISI
**Kupokelewa:** 30 Julai 2023
**Kurekebishwa:** 12 Nov. 2023
**Kukubaliwa:** 15 Des. 2023
**Kuchapishwa:** 29 Des. 2023
**Available at**
http://teku.ac.tz/article8.php

# Kanuni za Utokeaji wa Viambishi vya O-Rejeshi katika Lugha ya Kiswahili

Phides Kagwa

Idara ya Sanaa na Sayansi za Jamii, Chuo Kikuu Teofilo Kisanji, S.L.P 1104, Mbeya, Tanzania.
Mawasiliano: phideskagwa@yahoo.com, Simu: +255 (0) 748 887 532

**Ikisiri**

*Makala haya yanahusu kanuni za utokeaji wa viambishi vya O-rejeshi katika lugha ya Kiswahili hususan katika vitenzi na umbo la AMBA-. Mada hii itaongozwa na nadharia ya mashartizuizi katika mpangilio wa viambishi iliyoasisiwa na Bybee (1985) anasisitiza kuwa mpangilio wa viambishi huwa na uhusiano sawia, baina ya kiambishi kimoja na kingine. Pia, utokeaji wa viambishi hivyo huweza kutawaliwa na kanuni fulani, yaani viambishi hivyo havitokei kiholela hole bali hufuata kaida zinazotawala katika lugha husika. Hivyo, kuwepo kwa kiambishi {a} katika kitenzi husababisha kuwepo kwa kiambishi {b} katika kitenzi hicho. Wapo wataalamu mbalimbali wamejaribu kugusia suala la viambishi vya O-rejeshi katika lugha ya Kiswahili. Wataalamu hawa katika kutoa hoja zao kwa namna moja ama nyingine wamekinzana katika mazingira ya utokeaji wa viambishi hivyo kama ilivyojadiliwa na Kagwa (2021). Pia, hawakuweza kutoa kanuni zinazotalawa katika mazingira ya utokeaji wa viambishi vya O-rejeshi. Hivyo, Makala haya yataangazia kanuni zinazotawala mazingira ya utokeaji wa viambishi vya O-rejeshi katika vitenzi vya lugha ya Kiswahili huku tukiongozwa na nadharia ya Mashartizuizi.*

**Maneno Msingi:** Viambishi vya O-rejeshi, Mazingira ya Utokeaji, kanuni,Vitenzi vya Kiswahili, kabla na mzizi na baada ya mzizi neno.

## 1. Utangulizi

Viambishi vya O-rejeshi ni viambishi ambavyo huweza kutokea kabla na baada ya mzizi wa neno huku vikitanguliwa na kufuatiwa na viambishi mbalimbali na hutokea katika mazingira tofauti tofauti (Kagwa 2021). Wataalam mbalimbali waelezea namna ya utokeaji wa viambishi vya O-rejeshi kuwa huweza kutokea kabla na baada ya mzizi wa neno bila kuzingatia kanuni zinazotawala mazingira ya utokeaji wake na hawakutumia nadharia yoyote katika kuweka bayana kuhusu utokeaji wa viambishi hivi. Kwa mfano, Mekacha (1987), Wesana-Chomi (1991) na Saluhaya (2016) wanadai kuwa viambishi vya O-rejeshi hutokea kabla ya mzizi wa kitenzi na baada ya mzizi wa kitenzi na kupachikwa kwenye umbo AMBA-. Naye Polome (1967) anaeleza kuwa viambishi hivi huweza kujitokeza kwenye maumbo matatu tofauti ya vitenzi vya Kiswahili ambavyo ni vitenzi vyenye njeo, vitenzi visivyobeba njeo na vitenzi vya ukanushi. Pia, Kihore na wenzake (2009) wanadai kuwa viambishi vya O-rejeshi hutokea kabla ya mzizi wa neno. Wataalamu hawa japo wametupatia mwangaza wa kutambua kuwa katika lugha ya Kiswahili kuna viambishi vya O-rejeshi lakini hawakuenda mbali sana wao waliishia hapo bila kuzingatia kuwa viambishi hizi huweza kutawaliwa na kununi mbalimbali ambazo huweza kutokea katika mazingira mbalimbali kutokana na utokeaji wake. Hivyo, makala haya yameenda mbali zaidi na kuonesha kanuni zinazotawala mazingira ya utokeaji wa viambishi hivyo katika umbo la AMBA- na vitenzi vya lugha ya Kiswahili.

## 2. Tatizo

Viambishi vya O-rejeshi ni vipashio vya kiisimu ambavyo hupachikwa kabla na baada ya mzizi wa neno kwa kunzingatia mazingira maalumu ya utokeaji wake. Kwa kuzingatia kuwa baadhi ya maneno katika lugha ya Kiswahili hujengwa kwa viambishi mbalimbali ambavyo huwa na mpangilio maalumu na hutawaliwa na kanuni maalumu katika utokeaji wake, ni wazi kuwa ni vigumu kubaini mazingira halisi ya utokeaji wa viambishi vya O-rejeshi kwa kutumia matokeo jumuifu ambayo hayakubainisha kanuni yoyote yanayopatikana katika maadiko ya awali. Kwa mfano, kama viambishi vya O-rejeshi hutokea kabla ya mzizi, je hutokea kabla au baada ya viambishi vya nafsi na hutawaliwa na kanuni gani? Aidha, haijulikani kuwa viambishi vya O-rejeshi vinapotokea kabla na baada ya mzizi wa neno au kwenye umbo –AMBA hutawaliwa na kanuni zipi katika utokeaji wake. Katika mazingira haya, ni wazi kwamba linahitajika andiko litakaloweka bayana kanuni zinazotawala mazingira ya utokeaji wa viambishi vya O-rejeshi katika lugha ya Kiswahili.

Jinsi ya kuyarejea makala haya: Kagwa, P.. (2024). Kanuni za Utokeaji wa Viambishi vya O-Rejeshi katika Lugha ya Kiswahili. *TEKU Journal of Interdisciplinary Studies, 3*(2), 12–17 .

## 3. Kiunzi cha Nadharia

Makala haya yameongozwa na nadharia ya Mashariti Zuizi iliyoasisiwa na Bybee (1985). Nadharia hii inajikita katika msingi au kanuni ya mpangilio wa viambishi katika maneno kimofolojia. Inazingatia kuwa kuna kanuni maalumu ambazo zinafuatwa katika uundaji wa maneno. Manova na Aronoff (2010) wakishadidia hoja hii, wanaeleza kuwa mpangilio wa viambishi katika neno unatokea tu pale tunapounganisha viambishi kwa mpangilio maalumu na kupata umbo la neno. Mpangilio wa viambishi mara nyingi unajidhihirisha katika maneno kiulalo. Mpangilio huu hutawaliwa na kanuni. Kanuni hizo hueleza kwa nini kiambishi fulani kimepachikwa mahali fulani. Kwa mfano, neno lenye viambishi ABCDE, ambapo A,B,C,D, na E ni viambishi tofauti, mpangilio wa viambishi unatawaliwa na kanuni moja ya mazingira ya utokeaji inayoeleza kwa nini kiambishi A kimepachikwa pale na si sehemu nyingine. Kwa hiyo, Makala haya yameongozwa na nadharia hii ili kuelezea kanuni zinazotawala mazingira ya utokeaji wa viambishi vya O-rejeshi katika lugha ya Kiswahili.

## 4. Upatikanaji wa Data

Data zimepatikana kwa kutumia mbinu ya usomaji nyaraka. Nyaraka mbalimbali zilisomwa ili kusaidia kupata data toshelevu kwa ajili ya makala haya. Katika makala haya vimesomwa vitabu teule na kuteua maneno yenye viambishi vya O-rejeshi na kuyafanyia uchambuzi. Aidha, zimesomwa sura zote kwa kuruka ukurasa mmoja mmoja kwa upande wa tamthiliya na riwaya. Kwa upande wa ushairi ilitumika mbinu ya kuruka mashairi mawili mawili kutoka katika kitabu teule kwa kutumia mbinu ya usampulishaji nasibu taratibishi. Maneno yenye viambishi vya O-rejeshi yaliyokusanywa katika matini teule yalipangwa kisha viambishi vya O-rejeshi vilibainishwa ili kuweza kuvitolea ufafanuzi.

## 5. Kanuni Zinazotawala Utokeaji wa Viambishi vya O-rejeshi katika Vitenzi vya Lugha ya Kiswahili

Kagwa (2021) aliweza kubainisha mazingira mbalimbali ya utokeaji wa viambishi vya o- rejeshi katika maneno mbalimbali ya lugha ya Kiswahili ambapo, mazingira ya utokeaji yalifafanuliwa. Katika makala haya tutajikita katika kanuni zinazotawala utokeaji wa viambishi vya o-rejeshi katika vitenzi vya lugha ya Kiswahili kama zilivyobainika katika data hapo chini. Kanuni zinazotawala utokeaji wa viambishi katika neno zinaongozwa na nadharia ya masharti zuizi. Manova na Arano (2010) wanashadadia nadharia hii kuwa viambishi ambavyo vinapachikwa kwenye neno hutokea kwa kutawaliwa na kanuni fulani au kutotawaliwa na kanuni fulani. Kwa kutumia nguzo hii, viambishi vya o-rejeshi vilivyopachikwa katika mizizi ya maneno, vimechunguzwa utokeaji wake kwa kuvitenganisha na mzizi. Hivyo tukitumia kanuni hizo tunaweza kubaini viambishi hivyo vinavyotokea na kanuni zinazotawala utokeaji wake. Pia, Makala hii imebaini kuwa viambishi vya o-rejeshi hutokea kwa kutawaliwa na kanuni. Tofauti ya makala haya ni kwamba Polome (1967), Mekacha (1987) na Kihore na wenzake (2009) hawakugusia jambo la kanuni zinazotawala utokeaji wa viambishi vya o-rejeshi katika vitenzi vya Kiswahili. Ufuatao ni ufafanuzi kuhusu kanuni zinazotawala utokeaji wa viambishi vya o-rejeshi katika vitenzi vya lugha ya Kiswahili.

### 5.1. Kanuni Zinazotawala Mazingira ya Utokeaji wa Viambishi vya O-rejeshi katika Kiambishi AMBA-

Viambishi ambavyo vinapachikwa kwenye umbo la AMBA- hufuata kanuni maalumu. Viambishi hivyo mara zote hupachikwa baada ya umbo la AMBA- katika lugha ya Kiswahili. Kutokana kwamba kiambishi AMBA- ndicho kiambishi au mzizi pekee unaokubali viambishi vyote vya O-rejeshi, basi utokeaji wa viambishi O-rejeshi huwa na kanuni mbalimbali. Kanuni hizo zinajidhihirisha katika data ifuatayo:

a) Ambaye amba-**ye**
b) Ambao amba-**o**
c) Ambayo amba-**yo**
d) Ambako amba-**ko**
e) Ambalo amba-**lo**
f) Ambapo amba-**po**
g) Ambavyo amba-**vyo**
h) Ambazo amba-**zo**

Chanzo: Maktabani (vitabu vya *Kivuli Kinaishi*, *Chini ya Mwembe na Mirathi ya Hatari*).

Kielelezo 1: Kanuni Zinazotawala Mazingira ya Utokeaji wa Viambishi vya O-rejeshi katika Kambishi cha AMBA- katika Lugha ya Kiswahili

**{**O-rej} ⟶ {-ye} / AMBA —{Ngl 1 umoja}
**{**O-rej} ⟶ {-o} / AMBA —{Ngl 2 wingi, 3 umoja}
**{**O-rej} ⟶ {-yo}/ AMBA —{Ngl 4 wingi, 6 wingi}
**{**O-rej} ⟶ {-ko} / AMBA —{Ngl 18}
**{**O-rej} ⟶ {-lo} / AMBA —{Ngl 5 umoja}

Katika data hii viambishi vya O-rejeshi vinatawaliwa na kanuni tofauti. Kanuni hizo zinaweza kufafanuliwa kama ifuatavyo:

Kiambishi cha O-rejeshi {O} hutokea kama kiambishi cha O-rejeshi {-ye} katika, mazingira ya kutanguliwa na umbo la AMBA- ambapo kiima kinachoreje;ewa huwa katika ngeli ya kwanza umoja. Pia, kiambishi cha O-rejeshi {O} hutokea kama kiambishi cha O-rejeshi {-o} katika mazingira ya kutanguliwa na umbo la AMBA- ambapo kiima kinachorejelewa huwa katika ngeli ya pili wingi na ngeli ya tatu umoja. Vilevile, kiambishi cha O-rejeshi {o} hutokea kama kiambishi cha O-rejeshi {-yo} katika mazingira ya kutanguliwa na umbo la AMBA- ambapo kiima kinachorejelewa huwa katika ngeli ya nne wingi na ngeli ya sita wingi. Aidha, kiambishi cha O-rejeshi {o} hutokea kama kiambishi cha O-rejeshi {-ko} katika mazingira ya kutanguliwa na umbo la AMBA- ambapo kiima kinachorojelewa huwa katika ngeli ya kumi na nane na kiambishi cha O-rejeshi {O} hutokea kama kiambishi cha O-rejeshi {-lo} katika mazingira ya kutanguliwa na umbo la AMBA- ambapo kiima kinachorejelewa huwa katika ngeli ya tano umoja. Kwa ujumla ili viambishi vya O-rejeshi vitokee katika

umbo la AMBA- ni sharti vitabiliwe na ngeli za majina husika kama inavyoonekana katika kanuni hizo.

### 5.2. Kanuni Zinazotawala Mazingira ya Utokeaji wa Viambishi vya O-Rejeshi Vinavyo tokea Kabla ya Mizizi ya Vitenzi vya Uyakinishi vya Lugha Kiswahili

Viambishi vya O-rejeshi vinavyotokea kabla ya mzizi wa kitenzi cha uyakinishi utokea kwa kuzingatia kaida maalumu ambazo huweza kutofautiana na kaida za viambishi vya o-rejeshi vinavyotokea kabla ya mzizi wa kitenzi cha ukanushi. Kanuni hizi zimejidhihirisha katika data za utafiti kama zifuatazo;

(a) Zinazotawala zi-na-**zo**-tawal-a
(b) Aliyemsaidia a-li-ye-m-saidi-a
(c) Aliyosema a-li-**yo**-sem-a
(d) Wanaolazimika w a-na-**o**-lazim-ik-a
(e) Nilivyovikumbuka ni-li-vyo-vi-kumbu-k-a

**Chanzo:** Maktabani – Riwaya *Mirathi ya Hatari*

(Mung'ong'o, 1977) na tamthiliya ya *Kivuli Kinaishi* (Mohamed, 1990)

Kwa kutumia data hii, mazingira ya utokeaji wa viambishi vya O-rejeshi yanaweza kufafanuliwa kwa kanuni zifuatazo:

**{**O-rej} ⟶ {-zo} / {+id +nj} —{mzz} Ngl 10 wingi, 12 wingi
**{**O-rej} ⟶ {-zo} / {+id +nj} — ({ymb,kj}){mzz} Ngl 10 wingi na 12 wingi
**{**O-rej} ⟶ {-ye} / {+nfs +nj} {ymb) {mzz} Ngl 1umoja
**{**O-rej} ⟶ {-ye} / {+nfs +nj} —{ymb,kj} {mzz} Ngl 1umoja
**{**O-rej} ⟶ {-yo} / {+nfs +nj} —{mzz} Ngl 4wingi, 6wingi, 9umoja,14wingi
**{**O-rej} ⟶ {-yo} / {+nfs +nj} — ({ymb,kj}){mzz} Ngl 4wingi, 6wingi, 9umoja,14wingi
**{**O-rej} ⟶ {-o} / {+nfs +nj} {mzz} Ngl 2wingi, 3umoja, 9umoja,13umoja
**{**O-rej} ⟶ {-o} / {+nfs +nj} ({ymb,kj}) {mzz} Ngl 2wingi, 3umoja, 9umoja,13umoja
**{**O-rej} ⟶ {-vyo} / {+nfs +nj} {mzz} Ngl 8wingi
**{**O-rej} ⟶ {-vyo} / {+nfs +nj} ({ymb,kj}) {mzz} Ngl 8wingi

Kwa mujibu wa nadharia ya Masharti Zuizi, data hii inaonesha kuwa viambishi vya O-rejeshi vinapopachikwa kwenye mzizi wa kitenzi sharti vifuate kanuni maalumu. Kanuni hiyo imeelezwa katika utafiti huu kuwa, kiambishi cha O-rejeshi {O-rej} hutokea kama kiambishi cha O-rejeshi {-zo-} katika mazingira ya kutanguliwa na viambishi vya idadi na njeo na kufuatiwa na mzizi wa kitenzi ambapo kiima kinachorejelewa huwa katika ngeli ya 10 wingi na 12 wingi. Pia, kanuni ya jumla ya kiambishi cha O-rejeshi {-zo-} inakuwa, kiambishi cha O-rejeshi {O-rej} hutokea kama kiambishi cha O-rejeshi {-zo-} katika mazingira ya kutanguliwa na viambishi vya idadi na njeo na kuweza kufuatiwa na ama kiambishi cha yambwa au kujitendea na mzizi wa kitenzi ambapo kiima kinachorejelewa huwa katika ngeli ya ya 10 wingi na 12 wingi.

Pia, kiambishi cha O-rejeshi {O-rej} hutokea kama kiambishi cha O-rejeshi {-ye-} katika mazingira ya kutanguliwa na viambishi vya nafsi na njeo na kufuatiwa na yambwa na mzizi wa kitenzi ambapo kiima kinachorejelewa huwa na ngeli ya 1 umoja. Pia, kiambishi cha O-rejeshi {-ye-} huweza kuwa na kanuni ya jumla ambayo ni; kiambishi cha O-rejeshi {O-rej} hutokea kama kiambishi cha O-rejeshi {-ye-} katika mazingira ya kutanguliwa na viambishi vya nafsi na njeo na huweza kufuatiwa ama viambishi vya yambwa au kujitendea na mzizi wa kitenzi ambapo kiima kinachorejelewa huwa na ngeli ya 1 umoja. Aidha, kiambishi cha O-rejeshi {O-rej} hutokea kama kiambishi cha O-rejeshi {-yo} katika mazingira ya kutanguliwa na viambishi vya nafsi na njeo na kufuatiwa na mzizi wa kitenzi ambapo kiima kinachorejelewa huwa katika ngeli ya 4 wingi, 6 wingi, 9umoja, 14 wingi. Kanuni yake ya jumla ni kiambishi cha O-rejeshi {O-rej} hutokea kama kiambishi cha O-rejeshi {-yo-} katika mazingira ya kutanguliwa na viambishi vya nafsi na njeo na huweza kufuatiwa na viambishi vya yambwa au kujitendea na mzizi wa kitenzi ambapo kiima kinachorejelewa huwa katika ngeli ya 4 wingi, 6 wingi, 9umoja, 14 wingi.

Vilevile, kiambishi cha O-rejeshi {O-rej} hutokea kama kiambishi cha O-rejeshi {-o} katika mazingira ya kutanguliwa na viambishi vya nafsi na njeo na kufuatiwa na mzizi wa kitenzi ambapo kiima kinachorejelewa huwa katika ngeli ya 2 wingi, 3 umoja, 9 umoja na 13 umoja. Pia, kiambishi hiki huwa na kanuni yake ya jumla ambayo ni kiambishi cha O-rejeshi {O-rej} hutokea kama kiambishi cha O-rejeshi {-o} katika mazingira ya kutanguliwa na viambishi vya nafsi na njeo na kuweza kufuatiwa na viambishi vya yambwa au kujitendea na mzizi wa kitenzi ambapo kiima kinachorejelewa huwa katika ngeli ya 2 wingi, 3 umoja, 9 umoja na 13 umoja. Hata hivyo, kiambishi cha O-rejeshi {O-rej} hutokea kama kiambishi cha O-rejeshi {-vyo-} katika mazingira ya kutanguliwa na viambishi vya nafsi na njeo na kufuatiwa kiambishi cha yambwa na mzizi wa kitenzi ambapo kiima kinachorejelewa huwa katika ngeli ya 8 wingi. Aidha, kanuni ya jumla ya kiambishi cha O-rejeshi {-vyo-} ni kuwa kiambishi cha O-rejeshi {O-rej} hutokea kama kiambishi cha O-rejeshi {-vyo-} katika mazingira ya kutanguliwa na viambishi vya nafsi na njeo na kufuatiwa viambishi vya yambwa au kujitendea na mzizi wa kitenzi ambapo kiima kinachorejelewa huwa katika ngeli ya 8 wingi. Hivyo basi, kutokana na data ya 4.2.2 kanuni inaonesha kuwa ili kiambishi cha O-rejeshi kitokee katika kitenzi cha Kiswahili ni sharti kiwe na kiwakilishi cha ngeli za majina au nomino.

### 5.3 Kanuni Zinazotawala Utokeaji wa Viambishi vya O-Rejeshi Vinavyotokea baada ya Mzizi wa Kitenzi Yakinifu cha Kiswahili

Viambishi vya O-rejeshi vinavyotokea baada ya mzizi wa kitenzi yakinifu katika Kiswahili havitokei kiholela, bali hufuata kaida au utaratibu fulani katika utokeaji wake. Dai hili limejidhihirisha katika Makala haya. Zifuatazo ni data za viambishi vya O-rejeshi na kanuni zake:

1 Nitamkapo ni-tamk-a-**po**
2 Unipao u-ni-p-a-**o**
3 Wafikiapo wa-fik-i-a-**po**

4 Yaletwayo ya-let-w-a-**yo**
5 Yaamshayo ya-am-sh-a-**yo**

**Chanzo:** Maktabani:- Diwani ya *Chini ya Mwembe* (Ndumbaro na Gonsalves, 2017).

Katika data hii kanuni zinazotawala mazingira ya utokeaji wa viambishi vya O-rejeshi vinavyotokea baada ya mzizi wa kitenzi ni kama zifuatazo:

{O-rej} → {-po} / I tamati — ngl 16 Au

{O-rej} → {-po} / —# (T) ngl 16

{O-rej} → {-o} / I tamati — ngl 2 wingi,3 umoja, 11umoja, na 13 Au

{O-rej} → {-o} / # (T) ngl 2 wingi,3 umoja, 11umoja, na 13

{O-rej} → {-po} / I tamati — ngl 16 Au

{O-rej} → {-po} / — # (T) ngl 16

{O-rej} → {-yo} / I tamati — ngl 4wingi, 6wingi, 9 umoja na 14wingi Au

{O-rej} → {-yo} / — # (T) ngl 4wingi, 6wingi, 9 umoja na 14wingi

{O-rej} → {-yo} / I tamati — ngl 4wingi, 6wingi, 9 umoja na 14wingi Au

{O-rej} → {-yo} / — # (T) ngl 4wingi, 6wingi, 9 umoja na 14wingi

Katika data hii kiambishi cha O-rejeshi {O-rej} kinaonekana kujitokeza katika maumbo mbalimbali na mazingira sawa. Ujitokezaji wake wa namna hii unazingatia kanuni kama inavyoonekana hapo juu. Kwa mfano, katika data hii kiambishi cha O-rejeshi {O-rej} hutokea kama kiambishi cha O-rejeshi {-po} katika mazingira ya kutanguliwa irabu tamati au kutokea mwishoni mwa kitenzi ambapo kiima kinachorejelewa huwa katika ngeli ya 16.

Pia, kiambishi cha O-rejeshi {O-rej} hutokea kama kiambishi cha O-rejeshi {-o} katika mazingira ya kutanguliwa na irabu tamati au mwishoni mwa kitenzi ambapo kiima kinachorejelewa huwa katika ngeli ya 2 wingi, 3 umoja, 11umoja, 13. Kiambishi cha O-rejeshi {O-rej} hutokea kama kiambishi cha O-rejeshi {-yo} katika mazingira ya kutanguliwa na irabu tamati au mwishoni mwa kitenzi ambapo kiima kinachorejelewa huwa katika ngeli ya 4 wingi, 6 wingi, 9 umoja na 14 wingi. Hivyo basi, kitenzi kinapopokea kiambishi cha O-rejeshi baada ya mzizi, kwa ujumla, kitenzi hicho hakina uwezo wa kubeba viambishi vya njeo na ukanushi. Pia, hukifanya kitenzi kuonekana kipo katika hali ya mazoea mara zote.

### 5.4 Kanuni Zinazotawala Mazingira ya Utokeaji wa Viambishi vya O-rejeshi kabla ya Mizizi ya Vitenzi vya Ukanushi katika Lugha ya Kiswahili

Katika Makala ya Kagwa (2021) alibainisha mazingira ya utokeaji wa viambishi vya O-rejeshi vinavyotokea kabla ya mizizi ya vitenzi vya ukanushi katika lugha ya Kiswahili. Viambishi hivi katika vitenzi vya ukanushi katika lugha ya Kiswahili utokeaji wake hufuata kanuni maalumu. Kanuni hizo zinajidhihirisha katika data zifuatazo:

1 Asiyefahamu a-si-**ye**-faham-u
2 Isiyoweza i-si-**yo**-wez-a
3 Nisichokisikia ni-si-**cho**-ki-siki-a
4 Tusioielewa tu-si-**o**-i-elew-a
5 Asiyeniona a-si-**ye**-ni-on-a

**Chanzo:** Maktabani:- Riwaya *Mirathi ya Hatari* (Mung'ong'o,1977) na tamthiliya ya *Kivuli Kinaishi* (Mohamed, 1990)

Mazingira ya utokeaji wa viambishi vya O-rejeshi katika data ya 4.2.4 yanaweza kufafanuliwa kwa kanuni zifuatazo:

{O-rej} → {-ye-} / {+nfs +ukn} {mzz} ngl 1 umoja

{O-rej} → {-ye-} / {+nfs + ukn} — ({ymb, kj}) {mzz} ngl 1 umoja

{O-rej} → {-yo-} / {+nfs +ukn} —{mzz} ngl 4 wingi,6 wingi, 9umoja, 14

{O-rej} → {-yo-} / {+nfs +ukn} — ({ymb, kj}) {mzz} ngl 4 wingi,6 wingi, 9umoja, 14

{O-rej} → {-cho-} / {+nfs +ukn} —{ymb} {mzz} ngl 7 umoja

{O-rej} → { cho-} / {+nfs +ukn} — ({ymb, kj}) {mzz} ngl 7 umoja

{O-rej} → {-o-} / {+nfs +ukn} —{ymb} { mzz} ngl 2 wingi,3,11 umoja,13

{O-rej} → {-o-} / {+nfs +ukn} — ({ymb, kj}) { mzz} ngl 2 wingi,3,11 umoja,13

{O-rej} → {-ye-} / {+nfs +ukn} —{ymb} {mzz} ngl 1 umoja

{O-rej} → {-ye-} / {+nfs +ukn} — ({ymb, kj}) {mzz} ngl 1 umoja

Katika data hii kanuni zake zinaelezwa kama ifuatavyo: Kiambishi cha O-rejeshi {O-rej} hutokea kama kiambishi cha O-rejeshi {-ye-} katika mazingira ya kutanguliwa na viambishi vya nafsi na ukanushi na kufuatiwa na mzizi wa kitenzi ambapo kiima kinachorejelewa huwa katika ngeli ya 1 umoja. Kanuni yake ya jumla ni kuwa kiambishi cha O-rejeshi {O-rej} hutokea kama kiambishi cha O-rejeshi {-ye-} katika mazingira ya kutanguliwa na viambishi vya nafsi na ukanushina na kufuatiwa na viambishi vya yambwa au kujitendea na mzizi wa kitenzi ambapo kiima kinachorejelewa huwa katika ngeli ya 1 umoja Pia, kiambishi cha O-rejeshi {O-rej} hutokea kama kiambishi cha O-rejeshi {-yo-} katika mazingira ya kutanguliwa na viambishi vya nafsi na ukanushi na kufuatiwa na mzizi wa kitenzi ambapo kiima kinachorejelewa huwa katika ngeli ya 4 wingi, 6 wingi, 9 umoja na 14 wingi. Kanuni ya jumla ya kiambishi cha O-rejeshi {-yo-} ni kwamba kiambishi cha O-rejeshi {O-rej} hutokea kama kiambishi cha O-rejeshi {-yo-} katika mazingira ya kutanguliwa na viambishi vya nafsi na ukanushi na

kufuatiwa ama na kiambishi cha yambwa au kiambishi cha kijitendea na mzizi wa kitenzi ambapo kiima kinachorejelewa huwa katika ngeli ya 4 wingi, 6 wingi, 9 umoja na 14 wingi.

Aidha, kiambishi cha O-rejeshi {O-rej} hutokea kama kiambishi cha O-rejeshi {-cho-} katika mazingira ya kutanguliwa na viambishi vya nafsi na ukanushi na kufuatiwa na kiambishi cha yambwa na mzizi wa kitenzi ambapo kiima kinachorejelewa huwa katika ngeli ya 7 umoja. Pia, kiambishi cha O-rejeshi {-cho} kina kanuni ya jumla ambayo ni kiambishi cha O-rejeshi {O-rej} hutokea kama kiambishi cha O-rejeshi {-cho-} katika mazingira ya kutanguliwa na viambishi vya nafsi na ukanushi na kufuatiwa na viambishi vya yambwa au kujitendea na mzizi wa kitenzi ambapo kiima kinachorejelewa huwa katika ngeli ya 7 umoja. Kiambishi cha O-rejeshi {O-rej} hutokea kama kiambishi cha O-rejeshi {-o-} katika mazingira ya kutanguliwa na viambishi vya nafsi na ukanushi na kufuatiwa na kiambishi cha yambwa na mzizi wa kitenzi ambapo kiima kinachorejelewa huwa katika ngeli ya 2 wingi, 3 umoja, 11 umoja na 13 umoja.

Kanuni yake ya jumla ni, kiambishi cha O-rejeshi {O-rej} hutokea kama kiambishi cha O-rejeshi {-o-} katika mazingira ya kutanguliwa na viambishi vya nafsi na ukanushi na kufuatiwa na viambishi ama vya yambwa au kujitendea na mzizi wa kitenzi ambapo kiima kinachorejelewa huwa katika ngeli ya 2 wingi, 3 umoja, 11 umoja na 13 umoja. Kadhalika, kiambishi cha O-rejeshi {O-rejeshi} hutokea kama kiambishi cha O-rejeshi {-ye-} katika mazingira ya kutanguliwa na viambishi vya nafsi na ukanushi na kufuatiwa na kiambishi cha yambwa na mzizi wa kitenzi ambapo kiima kinachorejelewa huwa katika ngeli ya 1 umoja. Pia, kiambishi cha O-rejeshi {-ye-} huwa na kanuni ya jumla ambayo ni, kiambishi cha O-rejeshi {O} hutokea kama kiambishi cha O-rejeshi {-ye-} katika mazingira ya kutanguliwa na viambishi vya nafsi na ukanushi na kufuatiwa na kiambishi ama cha yambwa au kiambishi cha kujitendea na mzizi wa kitenzi ambapo kiima kinachorejelewa huwa katika ngeli ya 1 umoja. Vilevile, kiambishi cha ukanushi kinapopokea viambishi vya O-rejeshi hupoteza viambishi vya njeo na hali.

## 6.0 Hitimisho

Kwa kuzingatia kuwa makala haya yanahusu kanuni za utokeaji wa viambishi vya O-rejeshi katika lugha ya Kiswahili, imebainika kuwa viambishi vya O-rejeshi vya lugha ya Kiswahili havitokei kiholela bali hufauta kaida au kanuni mbalimbali kama zilivyoelezwa kwenye makala haya. Pia, viambishi hivyo hupangiliwa kwa utaratibu maalumu na mpangilo huo ndiyo hutabiri kanuni za utokeaji wa viambishi hivyo hii ni kutokanana na nadharia ya Masharti Zuizi inavyoeleza. Kuwapo kwa viambishi vya O-rejeshi katika vitenzi vya Kiswahili hutegemea kuwapo kwa viambishi vingine vilivyopangiliwa kama viambishi vya nafsi, njeo, yambwa na kwa mpangilio maalumu. Vilevile, utokeaji wa viambishi vya O-rejeshi hutabiliwa na ngeli iliyoambatana nayo katika neno husika. Hivyo, viambishi hivi hutokea pale umbo la AMBA- na vitenzi vinapoambatana na viambishi ngeli katika lugha ya Kiswahili. Aidha, Makala haya yanaonesha namna viambishi hivi kuwa vina kanuni tofauti za utokeaji yake, yaani kila kiambishi huwa na kanuni yake.


## Ufadhili

Hakuna.


## Migogoro ya Kimasilahi

Mwandishi wa Makala haya anatamka kwamba hakuna mgongano wa kimasilahi wowote utakaoweza kutokea kutokana na kuchapishwa kwa makala haya katika Jarida hili. Utafiti ulifanyika kwa jitihada za mwandishi mwenyewe pasipo malipo kutoka kwa mtu au shirika lolote.

## Marejeleo


Bybee, J. (1985). *Morphology: A study of the Relation between Meaning and Form*. Amsterdam: John Benjamins

Kagwa, P. (2021). "Mazingira ya Utokeaji wa Viambishi vya O-rejeshi katika Lugha ya Kiswahili." *TEKU Journal of Interdisciplinary Studies*, 1(2), 77-88.

Kihore na Wenzie (2009). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA): Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: TUKI.

Manova, S na Aronoff, M. (2010). Modeling Affix Order in Affix Combinations1. *Special issues of Morphology*, Manova, Aronoff (eds.). DOL: 10.1007/S11525-010-9153-6

Matinde, R.S. (2012). *Dafina ya Lugha Isimu na Nadharia*. *Kwa Sekondari, Vyuo vya Kati na Vyuo Vikuu.* Mwanza: Serengeti Educational Publishers.

Mekacha, R.D.K. (1987). "Tungo Rejeshi katika Tungo za Kiswahili". *Mulika*, *19*, 83–91.

Mohamed, S. A. (1990). *Kivuli Kinaishi*. Nairobi: Oxford University Press.

Mung'ong'o, C. G. (1977). *Mirathi ya Hatari*. Dar es Sa laam: Mkuki na Nyota.

Ndumbaro, E. na Gonslves. G. (2017). *Chini ya Mwembe: Kusanyiko la Mashairi*. Dar es Salaam: Green Earth Paper Products.

Polome, C.E. (1967). *Swahili Language Handbook*. Printed United State of America.

Saluhaya, M.C. (2016). *Nadharia ya Lugha: Kidato cha Tano, Sita na Elimu ya Juu*. Dar es Salaam: Ahmadiya.

Wesana-Chomi, E. (1991) Sarufi Tangulizi ya Kiswahili. Haijachapishwa.

## Wasifu wa Mwandishi



Jina langu ni **PHIDES KAGWA**, mzaliwa wa mkoa wa Kagera wilaya ya Muleba kata ya Nshamba, na kijiji cha Bunyagongo. Nilisoma shule ya msingi Bunyagongo kuanzia mwaka 1996—2002. Mwaka 2003—2006 nilisoma shule ya sekondari Biirabo iliyopo wilayani Muleba na 2007 nilisoma shule ya sekondari Rulenge iliyopo wilayani Ngara. Pia, mwaka 2009—2011 nilisoma shule ya sekondari ya Wasichana Kowak iliyopo wilayani Rolya. Mwaka 2011/2012—2014 nilisoma shahada ya awali chuo kikuu cha Dar es Salaam na shahada ya umahili nilisoma 2016/2017—2019 Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Mwaka 2020 niliajiriwa Chuo Kikuu Teofilo Kisanji (TEKU) kama mhadhiri msaidizi katika Lugha ya Kiswahili mpaka sasa.

Jinsi ya kuyarejea makala haya: Kagwa, P.. (2024). Kanuni za Utokeaji wa Viambishi vya O-Rejeshi katika Lugha ya Kiswahili. *TEKU Journal of Interdisciplinary Studies, 3*(2), 12–17 .